



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA



**TANGAZO LA KUHUISHA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI
MIRADI YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NA WATAALAMU
ELEKEZI WA MAZINGIRA**

Ibara ya 17 ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imeainisha madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa sera na sheria ya mazingira. Pamoja na masuala mengine Baraza limepewa majukumu ya kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Wataalam Elekezi wa Mazingira. Majukumu haya yanahusisha kuratibu, kufanya mapitio ya taarifa za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji. Aidha, Ibara ya 83 ya Sheria ya Mazingira imeanisha kuwa TAM itafanywa na Mshauri Elekezi wa Mazingira ambaye jina lake pamoja na taaluma imesajiliwa na Baraza.

Hivyo, katika kuboresha mfumo yake ya mapitio ya taarifa za tathmini na kaguzi za athari za mazingira na usajili wa Wataalam Elekezi wa Mazingira, Baraza limeboresha miundo mbinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kulingana na matakwa ya Mfumo wa Serikali Mtandao (e-Government). Hivyo, mnafahamishwa ya kuwa Baraza limeboresha mfumo wa kielektroniki wa kusajili Miradi ya Tathmini za Mazingira na Ukaguzi (*Online Registration and Tracking System*) kwa kuongeza usajili wa Wataalam Elekezi kielektroniki na kipengele kitakacho wezesha Wataalam Elekezi kufanyia kazi miradi ya TAM katika akaunti zao wenyewe.

Mfumo huu utatumia na makundi husika kama ifuatavyo:

- i. Waandaaji wa Miradi kusajili mradi;
- ii. Wataalam Elekezi wa Mazingira kuomba usajili na kufanyia kazi miradi ya TAM
- iii. Watumishi wa Baraza kupokea na kufanyia kazi maombi yanayowasilishwa ya TAM; na
- iv. Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) watatumia mfumo huu kufanyia kazi maombi ya TAM kabla ya Waziri kuidhinisha utekelezaji wa miradi.

Mfumo huu ni mahususi katika jitihada zinazofanywa na Baraza za kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha mazingira bora na wezeshi kwa wawekezaji hususani walio na lengo la kuanzisha shughuli za maendeleo. Hivyo basi, mfumo huu unakusudiwa kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi na pia kulisaidia Baraza kuwa na kumbukumbu za uhakika katika masuala yanayohusu miradi na usimamizi wa mazingira. Aidha, malipo yote ikiwa ni pamoja na gharama za usajili wa miradi na Wataalam Elekezi, na gharama za mapitio ya miradi yanafanyika kwa mfumo wa malipo wa serikali wa kielektroniki ikiwa ni

pamoja na kupata hati ya madai (invoice) na kumbukumbu namba ya malipo (control number).

Mfumo huu unapatikana kwenye tovuti za Baraza kutokana na kundi husika kama ilivyoainishwa hapa chini:

- i. Waandaaji wa Miradi na Wataalam Elekezi wa Mazingira (*eia.nemc.or.tz*);**
- ii. Watumishi wa Baraza (*pms.nemc.or.tz*); na**
- iii. Watumishi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (*vpo.nemc.or.tz*).**

Kwa misingi hiyo na kuufanya mfumo huo utumike, taasisi zote nchini, wawekezaji, wataalam elekezi, wananchi na wadau wote wa mazingira mnataarifiwa kuwa mfumo huo utaanza rasmi tarehe 3rd april 2022 ambapo usajili wa wataalam elekezi utafanyika kwa mfumo wa kieletroniki.

Pamoja na kuhuisha mfumo huo, miradi ya tathmini ya athari kwa mazingira (TAM) utaendelea kutafanyika kwa mfumo wa kielektroniki kama ilivyo sasa. Hata hivyo, Baraza linatahadharisha maboresho hayo yanaweza kupelekea mfumo kutopatikana kabisa au kukatika kwa kipindi kifupi.

Kwa msaada unaweza kuwasiliana nasi kupitia eiasupport@nemc.or.tz au tembelea tovuti ya Baraza (nemc.or.tz) au tembelea Ofisi za Makao Makuu ya Baraza zilizopo katika kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent, Mikocheni katika ofisi za kanda za Baraza zilizopo Arusha, Dodoma, Mbeya, Kigoma, Mwanza na Mtwara.